
Ufugaji wa nguruwe hapa nchini umeanza siku nyingi hususani katika mikoa ya nyanda za juu kusini (Mbeya, Rukwa, Iringa, na Ruvuma), Kaskazini (Manyara, Arusha, na Kilimanjaro). Aina za nguruwe wanaofugwa hapa nchini ni wa kigeni, chotara na koo mbalimbali za kienyeji.

Zifuatazo ni aina za nguruwe wanaopatikana hapa Tanzania:-




**1.Nguruwe wa Kigeni**



1. large white

- Asili yake ni Uingereza
- Ana rangi nyeupe katika ngozi na manyoya
- Ana masikio yaliosimama, paji la uso lililoingia ndani kama bakuli
- Ana mwili mrefu mnene
- Ana tumbo kubwa, mzito na miguu yenye nguvu
- Ana uwezo wa kukua haraka na kuzalisha nyama isiyo na mafuta akiwa na umri mdogo
- Ana uwezo mkubwa wa kuzaa watoto wengi kwa mzao
- Ni mpole na ana uwezo mkubwa wa kutunza watoto
- Jike ana uwezo wa kutoa maziwa mengi.

2. Landrace



- Asili yake ni Denmark
- Ana rangi nyeupe na ni mrefu mwembamba
- Masikio yake ni makubwa na yamesimama kwa mbele na mara nyingi hufunika macho
- Ana kichwa kidogo na shingo nyembamba ukilinganisha na ukubwa wa mwili
- Ana uwezo wa kuzaa watoto wengi kwa mzao
- Ana uwezo wa kukua haraka na kuzalisha nyama isiyokuwa na mafuta mengi

3.Wessex saddleback



- Asili yake ni uingereza
- Ana rangi nyeusi na nyeupe mfano wa mkanda kuzunguka mabega na miguu ya mbele
- Ni mfupi na masikio yameinama kwa mbele
- Ana mgongo uliopinda mfano wa upinde
- Ana uwezo wa kutoa maziwa mengi na kutunza watoto.

4.Hampshire



- Asili yake ni marekani
- Ana rangi nyeusi na rangi nyeupe mfano wa mkanda kuzunguka mabega, kifua na miguu ya mbele
- Ni mfupi na masikio yamesimama
- Ana mgongo uliopinda kidogo mfano wa upinde
- Ana uwezo wa kuzaa watoto wengi na kuwatunza

**2. Nguruwe chotara**



- Ni uzao unaotokana na kupandisha nguruwe wa aina tofauti kwa mfano nguruwe wa kienyeji akipandishwa na wa kigeni (kisasa)
- Hustaimili magonjwa ukilinganisha na nguruwe wa kienyeji

**3.Nguruwe wa kienyeji**



- Huwa na rangi tofauti
- Huwa ni wadogo kwa umbo
- Hukua taratibu
- Wana uwezo wa kustaimili mazingira magumu
- Nyama yake haina mafuta mengi
- Wana uwezo wa kujitafutia chakula

UTUNZAJI WA NGURUWE DUME

Utunzaji wa nguruwe mara nyingi hutegemea aina ya makundi ya nguruwe na mfunmo wa ufugaji. Makundi ya nguruwe ni kama madume ya mbegu, majike wazazi, watoto, na wale wanaonenepeshwa kwa ajili ya nyama au mafuta. Nguruwe wanaweza kufugwa ndani au nje ya banda, kutegemea na ukubwa wa shamba, kipato kilichopo kwa shughuli za ufugaji.

Ili kuleta mafanikio na tija katika ufugaji wa nguruwe ni vema kuzingatia utunzaji bora ikiwa ni pamoja na aina ya banda, uchaguzi wa nguruwe wazazi, ulishaji, udhibiti wa magonjwa na uangalizi kwa ujumla.

## 1.0 Utunzaji wa dume la Mbegu

utunzaji bora wa dume unaanza kwa kuchagua dume bora kwa ajili ya uzalishaji. Uchaguzi wa dume la kuzalisha ni muhimu kuliko uchaguzi wa jike kwa sababu dume moja hutumika kuzalisha nguruwe wengi katika kundi.
1.1 Uchaguzi wa Dume bora
Wakati wa kuchagua dume mfugaji anashauriwa kuzingatia yafuatayo:-

- Achaguliwe kutoka kwenye koo wenye historia ya kukua haraka, kukuza watoto wengi na kuwatunza, kutokuwa na magonjwa au kilema cha kurithi.
- Awe na miguu imara, mchangamfu na mwenye afya bora
- Awe na umbile zuri linaloendana na aina yake na misuli imara itakayomwezesha kuoanda bila matatizo
- Awe na kende mbili, kubwa, zilizokamilika na zinazolingana
- Awe anayekua haraka na mwenye uwezo mkubwa wa kubadili chakula kwa matumizi ya mwili kuwa nyama
- Awe na chuchu zisizopungua 12
- Asiwe na mahisiano ya kinasaba (kama kaka na dada, mtoto na mama au mtoto na baba) na maike anayotegemea kuyapanda
- Awe mrefu na mgongo ulionyooka

## 1.1 Ulishaji wa dume

Dume kwa ajili ya kupandisha apewe chakula bora chenye viini lishe vya kutosha vitakavyotosheleza mahitaji ya mwili bila kumfanya mnene sana au kukonda. Wakati wa msimu wa upandishaji alishwe chakula bora kiasi cha kilo 2.7 hadi 3.6 kwa siku. Wakati ambao sio msimu wa kupandisha, dume apewe chakula bora kiasi cha kilo 2 kwa siku. Kwa matumizi mazuri ya chakula hicho kigawanywe na kulishwa mara mbili kwa siku. Pia inatakiwa dume apewe maji safi na salama ya kutosha kila siku wakati wote.

## 1.2 kinga dhidi ya Magonjwa na Wadudu

Uzuiaji wa magonjwa na wadudu ni muhimu kwa afya ya nguruwe dume. Mfugaji anashauriwa kumwona mtaalam wa mifugo aliyekaribu nae ili kupata ushauri juu ya chanjo muhimu ka ajili

kuzuia magonjwa kwa wanyama wake. Mfano kwenye sehemu ambazo ndorobo, mfugaji anashauriwa kutumia chanjo.

Kuzuia wadudu, mfugaji anashauriwa kuogesha nguruwe kwa dawa za kuogeshea angalau mara mbili kwa wiki ili kuzuia ukurutu na matatizo mengine ya ngozi. Kuzuia minyoo mfugaji anashauriwa kuwapa dawa ya minyoo kila baada ya miezi mitatu. Ni muhimu banda, vifaa vya kulishia na kunyweshea maji viwe safi wakati wote.

### 1.3 Utaratibu a kutumia Nguruwe dume kupanda

Upandishaji wa nguruwe unaweza kufanyika kwa njia mbili, ya kutumia dume au uhamilishaji. Njia ya kutumia dumendio inayotumiaka hapa nchni kwa utaratibu ufuatao:-

- Nguruwe dume aruhusiwe kupanda kwa mara ya kwanza akiwa na umri wa miezi nane hadi kumi
- Akiwa na umri wa miezi 10 hadi 18 anaruhusiwa kupanda mara moja kwa wiki
- Akiwa na miezi 18 hadi 24 anaruhusiwa kupanda mara nne hadi tano kwa wiki
- Dume wakubwa wasitumike kupanda majike wadogo kwani wanaweza kuleta madhara kama vile kuwavunja migongo.
- Dume aruhusiwe kuendelea kupanda mpaka umri wa miaka 5 hadi 6

Mfugaji anashauriwa kuwa, ni muhimu dume la kupandisha liwekwe kwenye chumba chenye eneo la mita za eneo 9.3 ili kuweza kupata mazoezi ya mwili ikiwa sehemu ya kupanda imetenganishwa eneo liwe la mita mraba saba. Madume yatenganishwe na Majike ili kuepusha kupanda wakati usiotakiwa.

UTUNZAJI WA NGURUWE JIKE

Utunzaji bora wa majike ni muhimu kwani utamuwezesha mfugaji kupata Mawazo mengi na bora.Majike azazi watunzwe vizuri ili kuongeza idadi Ya watoto watakaozaliwa kwa mwaka na kuongeza faida kwa mfugaji. Utunzaji bora ni kiini cha idadi ya watoto watakaozaliwa,watakaoishi na Muda wataochukua kufikia uzito kuuza na gharama zitakazotumika.

**Kuchagua jike Bora**
Mfugaji anashauriwa kuchagua nguruwe jike anayetegemewa kuwa mzazi kwa kuzingatia sifa zifuatazo:-

- •Awe amezaliwa na mama anayezaa watot wengi,menye kutoa maziwa mengi na mtunzaji mzuri wa watoto
- • Awe na afya nzuri
- • Awe na kiwele kikubwa chenye chuchu kati ya 10 hadi 14
- • Awe ni MRE na mwenye uwiano mzuri kati ya urefu, upana na kimo
- • Awe na umbile la kumuwezesha kubeba mimba na kuzaa kwa urahisi
- • Awe na miguu imara iliyonyooka,kwato imara,mgongo wenye nguvu na uliopinda kiasi
- • Awe mpole
- • Atokane na wazazi wasiokuwa na historia ya magonjwa au klema cha kurithi.

**Taratibu za kupandisha majike**

Nguruwe kike anaanza kuonyesha dalili za joto akiwana umri wa miezi sitahadi saba.Hata hivyo, inasshauriwa kutompandisha kipindi hicho ili kuzuia kuzaliwa watoto wenye uzito mdogo,kupata mtatizo wakati wa kuzaa,afya mbaya na kudumaa. Hivyo, inapendekezwa nguruwe apandishwe atakapoonyesha dalili za joto kwa mara ya pili au ya tatu.

Kwa kawaida nguruwe huwa tayari kupandishwaakiwa na umri wa miezi kati ya nane na tisa kutegemea afya na aina ya nguruwe.

**Kumtambua Nguruwe Aliye Kwenye Joto**
Mfugaji anashauriwa kuwachunguza nguruwe siochini ya mara mbili kwa siku hususani asubuhi na jioni wakati wa kuwalisha ili kutambua dalili za joto.

**Zifuatazo ni daliliza nguruwe jike aliye kwenye joto**

- • Hupoteza hamu ya kula
- • Hutoa sauti ya kugugumia
- • Huhangaika mara kwa mara
- • Hupandwa na wenzake na hutulia akipandwa au akigandamizwa mgongoni

- •   Sehemu ya uke huvimba na huwa nyekundu
- •   Hukojoa mara kwa mara na hutoa ute
- •   Husimama wima na hutulia akiwa ametanua miguu ya nyuma na mkia ukielekea juu wakati akipandwa na dume.

Dalili hizi sio lazima zionekane zote wakati mmoja hivyo ni jambo la muhimu kuwa mwangalifu.Ili dalili hizi ziweze kuonekana vizuri,chumba cha majike yanayotarajiwa kupandwakinatakiwa kiwe karibu na cha dume.
Joto hudumu kwamuda wa sikumbili hadi tatu.Nguruwe jike apandishwe mara mbili kwa siku hususani asubuhi na jioni.Nguruwe apandishwe masaa 12 hadi 24 anapoonyesha dalili za kusimama akipandwa na dume au akigandamizwa mgongoni.Kwa kawaida nguruwe hurudia kuingia kwenye joto kila baada ya siku 21 ikiwa hana mimba.Mfugaji anashsuriwa kumchunguza ngurwe jike baada ya kumpandisha aingia kwenye joto baada ya kupandishwa. Wakati wa kupandisha inashauriwa nguruwe jike kupelekwa kwenye chumba cha dume ili kuzuia dume kushambuliwa na jike.Nguruwe ambaye hashiki mimba baada ya kupandishwamara nyingi inashauriwa mfugaji kumuona Daktari wa mifugo kwa ushauri.

**Ulishaji wa jike**
Kabla ya kupandishwa nguruwe jike apewe kilo 2.5 hadi 3 za chakula kwa siku na kupewa maji safi na ya kutosha wakati wote.

**Kutunza Nguruwe Wenye Mimba**
Utunzaji bora wa nguruwe wenye mimba ni muhimu katika kupata watoto wenye uzito mkubwa na afya bora.Pia husaidia nguruwe kuwa na afya bora,kutoa maziwa mengi nakupunguza vifo vya watoto.
Mimba ya nguruwe huchukua siku 114hadi 119(miezi mitatu,wiki tatu na siku tatu) hadi kuzaa.Kwa kipindi hicho nguruwe anahitaj lishe bora na maji,hewa safi nay a kutosha, mazoezi pamoja na kinga dhidi ya magonjwa.Hivyo, inashauriwa banda liwe na nafasi ya kutosha, na safi muda wote.

**Ulishaji wa Nguruwe Wenye Mimba**

Nguruwe mwenye mimba anahitaji kupewa cha kula kinacholeta nguvu na kujenga mwili. Inashauriwa, mwezi wa kwanza wa umri wa mimba apewe kilo 2 hadi 2.5 kwa nguruwe mwenye afya nzuri, akiwa dhaifu apewe kilo 3 kwa majuma matatu. Pia, baada ya siku 84 za umri wa mimba apewe kilo 2 za chakula kwa siku na kuongeza nusu klo kila wiki mpaka siku ya tatu kabla ya kuzaa. Siku tatu kabla ya kuzaa, chakula kipunguzwe hadi kufikia kilo 2 kwa siku na wapewe majani kama luseni au chakula chenye nyuzi nyuzi nyingi kama pumba kilo moja kwa siku tatu kabla ya kuzaa ili kuzuia tatizo la kinyesi kuwa kigumu ambacho hushindwa kutoka na kusababisha nguruwe kuzaa kwa shida. Siku ya kuzaa nguruwe asipewe chakula apewe maji tuu.

**kinga dhidi ya Maginjwa na Wadudu**

Nguruwe wenye mimba huathiriwa zaidi na minyoo na magonjwa mengine. Minyoo hupunguza hamu ya kula na hivyo huathiri afya ya nguruwe pamoja na ukuaji wa mimba. Uzuiaji wa magonjwa na wadudu ni muhumu kwa afya ya nguruwe mwenye mimba. Mfugaji anashauriwa kuwapa nguruwe dawa ya kuzuia minyoo siku 21 hadi 28 kabla ya kuzaa.

Kuzuia wadudu, mfugaji anashauriwa kuogesha kwa dawa zakuogeshea angalau mara mbili kwa wiki ili kuzuia ukurutu na matatizo mengine ya ngozi. kwenye sehemu ambazo kuna ndorobo, mfugaji anashauriwa kuwachanja nguruwe. Ni muhimu banda na vifaa vya kulishia na maji viwe safi wakati wote.

Source:

http://ujasiliamali01.blogspot.com/2016/08/utunzaji-wa-nguruwe-jike.html

Accessed on 27/12/2019